**RIPOTI YA TATHMINI YA CAO**

**Kuhusu Malalamishi Kuhusiana na Uwekezaji wa IFC kwenye Kampuni za Delonex Energy na Africa Oil (#33557 na #36699) nchini Kenya**

Oktoba 2020

Afisi ya Compliance Advisor Ombudsman
*kwa niaba ya*
Shirika la Fedha la Kimataifa na
Wakala wa Dhamana ya Uwekezaji wa Wahusika Anuwai
**www.cao-ombudsman.org**

## Kuhusu CAO

Afisi ya Compliance Advisor Ombudsman (CAO) ni utaratibu wa uwajibikaji unaojisimamia wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC) na Wakala wa Dhamana ya Uwekezaji wa Wahusika Anuwai (MIGA), matawi ya kibinafsi ya Benki ya Dunia. CAO inaripoti moja kwa moja kwa Rais wa Benki ya Dunia, na wajibu wake ni kusaidia kutatua malalamishi kutoka kwa waathirika wa miradi iliyodhaminiwa na IFC/MIGA kwa njia ya haki, isiyo na upendeleo na ya kutoa maoni yanayosaidia, ili kuimarisha matokeo kwa jamii na kwa mazingira ya miradi hiyo.

Kupata maelezo zaidi, zuru www.cao-ombudsman.org

## YALIYOMO

YALIYOMO ........ III
ORODHA YA AKRONIMU ........ IV
1. MAELEZO YA JUMLA ........ 1
2. USULI ........ 1
   2.1 Miradi ya IFC ........ 1
   2.2 Malalamishi ........ 2
3. MUHTASARI WA TATHMINI ........ 3
   3.1 Methodolojia ........ 3
   3.2 Muhtasari wa Maoni ........ 3
4. HATUA ZINAZOFUATA ........ 10
KIAMBATISHO A. MAONI YA TULLOW ........ 11
KIAMBATISHO A. UTARATIBU UNAFUATWA NA CAO KUSHUGHULIKIA MALALAMISHI ........ 14

## ORODHA YA AKRONIMU

| | |
|---|---|
| AOC | Shirika la Africa Oil Corp |
| CAO | Afisi ya Compliance Advisor Ombudsman |
| CLO | Afisa wa Uhusiano Mwema na Jamii |
| Delonex | Kampuni ya Delonex Energy UK Limited |
| ESIA | Ripoti ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na kwa Jamii |
| IFC | Shirika la Fedha Duniani |
| JCAP | Mradi wa Haki na Uwajibishaji wa Kampuni (JCAP) |
| KVCO | Muungano wa Jamii za Kerio Valley |
| MIGA | Wakala wa Dhamana ya Uwekezaji wa Wahusika Anuwai |
| NEMA | Mamlaka ya Kitaifa Inayosimamia Mazingira |
| Tullow | Kampuni ya Tullow Kenya B.V |

# 1. MAELEZO YA JUMLA

Mnamo Agosti mwaka wa 2019, CAO ilipokea malalamishi kutoka kwa wanajamii wanaoishi katika kaunti za Baringo, Elgeyo Marakwet, na Pokot Magharibi nchini Kenya wakisaidiwa na shirika ya uraia linalopatikana nchini Kenya na shiriks linaloshughulikia sheria linalopatikana nchini Canada. Malalamishi yanahusu athari zinazotokana na shughuli za utafiti wa kijiolojia unaolenga kutafuta mafuta na gesi uliofanyika katika Block 12A (Mradi), eneo la zaidi ya kilomita 15,000 mraba na linalojumuisha kaunti za Elgeyo Marakwet, Baringo, Pokot Magharibi, Turkana, na Samburu nchini Kenya. IFC inaendesha miradi miwili inayohususiana na Block 12A, mojawapo na kampuni ya Delonex Kenya (One) Limited na mwingine na kampuni ya Africa Oil Corp, kampuni zilizojishughulisha na Block 12A tangu mwaka wa 2010 hadi mwaka wa 2017. Ijapokuwa kampuni ya Africa Oil Corp imesitisha shughuli zake katika Block 12A, Africa Oil Corp kama kampuni, bado inapokea ufadhili kutoka kwa IFC.

Mnamo Septemba mwaka wa 2019, CAO ilibaini kuwa malamishi hayo yalikidhi vigezo vyote vitatu vya utaratibu uliowekwa kuwezesha malalamishi kukubalika. Wakati wa tathmini ya malalamishi iliyofanywa na CAO, kampuni ya Delonex na Walalamishi waliamua kushughulikia malalamishi yaliyotolewa kupitia mchakato wa utatuzi wa mzozo unaondeshwa na CAO. Kampuni ya Africa Oil ilisema kuwa haitashiriki kwenye mchakato huu.

Mchakato wa tathmini ulichukua mda zaidi kuliko mda wa kawaida wa siku 120 za kufanya kazi. Hii ilitokana na haja ya kutafuta kampuni ya Tullow Kenya B.V., iliyoendesha shughuli zake hapo awali kwenye Block 12A, iliyotajwa wakati wa tathmini. Kampuni ya Tullow Oil ilitoa maoni yake kwa CAO kuhusiana na malalamishi na ikauliza yajumuishwe kwenye ripoti. Pia, ilionyesha kuwa kulikuwa na uwezekano wa wao kushiriki kama mwangalizi katika majadiliano kati ya Walamishi na Delonex yatakayoongozwa na CAO, iwapo wahusika wataafikiana kuhusu kanuni zitakazoyaongoza.

# 2. USULI

## 2.1 Miradi ya IFC

Miradi miwili ya IFC inayohusu Block 12A inatekelezwa na kampuni ya Delonex Kenya (One) Limited (Delonex) na Africa Oil Corp (AOC). Miradi yote miwili bado inaendelea.

Kulingana na taarifa walizonazo IFC, IFC ilifanya ingewekeza hisa za mtaji zenye thamani ya dola za Marekani milioni 60 kwenye kampuni ya Delonex katika mwaka wa 2013 ili kuwezesha utafiti wa kijiolojia na kuwezesha Delonex kujipatia vifaa vilivyohitajika kutumiwa kutafuta mafuta na gesi katika maeneo ya Afrika Mashiriki na Afrika ya Kati.[1] Kwa kuongezea, katika mwaka wa 2015, IFC ilifanya uwekezaji wa hisa za mtaji wa dola za Marekani milioni 50 katika kampuni ya AOC ili kuwezesha shughuli za utafiti wa kijiolojia na tathmini zinazolenga kutafuta mafuta na gesi, na kutoa mtaji wa jumla unahitajika kuendeleza kazi yao kwenye block 10BB na block 13T Kusini mwa Lokichar. IFC bado imewekeza hisa za mtaji katika kampuni ya AOC. Miradi hiyo yote inaorodheshwa chini ya Kundi A la Mazingira na IFC.[2]


Wakati wa mchakato wa tathmini, AOC ilisema kuwa ijapokuwa walikuwa na nia ya kushiriki kwenye Mradi huo tangu mwaka wa 2010 hadi mwaka wa 2017, hawakuendeleza shughuli zozote kwenye Block 12A, na kuwa kampuni ya Tullow Kenya B.V. (Tullow) ndiyo

[1] Tembelea wavuti wa 'IFC Disclosure Website' , Maelezo kuhusu Mradi (Project Description), kupitia https://disclosures.ifc.org/#/projectDetail/SII/33557

[2] Tembelea wavuti wa 'IFC Disclosure Website' , Project Description, kupitiahttps://disclosures.ifc.org/#/projectDetail/SII/36699

iliyoendelesha mradi. Hii ni kutokana na kutia sahihi Makubaliano ya Kuendesha Mradi Pamoja kati ya Tullow na AOC waliotia sahihi mwaka wa 2011. Delonex walisema kuwa walimiliki hisa kwa Block 12A mnamo Septemba mwaka wa 2015 na kuendesha mradi huo na kampuni ya Tullow katika mwezi wa Januari mwaka wa 2018. IFC ilikiri kuwa haikufadhili shughuli za Tullow katika Block 12A. Kurahisisha kazi, Mchoro wa kwanza hapo chini unaonyesha mradi huo na waendeshaji tofautitofauti wa Mradi huo.

**Mchoro wa Kwanza**




## 2.2 Malalamishi

Mnamo Agosti mwaka wa 2019, CAO ilipokea malalamishi kutoka kwa wanajamii wapatao 140 kutoka katika kaunti za Baringo, Elgeyo Marakwet na Pokot Magharibi ("Walalamishi"). Malalamishi hayo yaliungwa mkono na Muungano wa Jamii ya Kerio Valley (KVCO), shirika la uraia nchini Kenya na Mradi wa Haki na Uwajibishaji wa Kampuni (JCAP), shirika linaloshughulikia masuala ya sheria lililo na makao yake makuu nchini Canada. Malalamishi hayo yanahusu kutokuwa na taarifa kuhusiana na Mradi na kutoshauriana na washikadau kuhusiana na mradi huo, kushindwa kushughulikia madhara kutokana na mradi huo, uvunjaji wa kanuni za Mfumo wa Kudumu wa IFC, na athari kwa ardhi, kwa kipato na kwa mazingira.

Masuala yaliyoibuka wakati wa tathmini yanaelezwa kwa kina katika sehemu ya tatu inayofuata ya ripoti hii.

## 3. MUHTASARI WA TATHMINI

### 3.1 Methodolojia

Nia ya tathmini iliyofanywa na CAO ni kuelewa vizuri malalamishi na masuala yaliyoibuliwa na Walalamishi kupitia ukusanyaji wa taarifa kutoka kwa washikadau bila kutoa uamuzi kuhusu iwapo malalamishi yanatambuliwa au la. Tathmini hii pia inalenga kubainisha ni mchakato upi wa CAO ambao Walalamishi na Mteja/Wateja wa IFC wangependa kutumia—mchakato wa Utatuzi wa Mzozo, au mchakato wa Ridhaa (tazama Kiambatisho A kuona hatua ambazo CAO hutumia kutatua mzozo).

Hapa, tathmini ya malalamishi iliyofanywa na CAO ilihusisha:

- uhakiki wa nyaraka kuhusu uwekezaji wa IFC katika kampuni za Delonex na AOC;
- mikutano ya ana kwa ana na Walalamishi 40 mjini Eldoret na Cheptebo (baadhi yao wakijiwakilisha, baadhi yao walidai kuwa walikuwa wanawakilisha jamii yao);
- kuzuru nyumba za Mlalamishi aliyelalamika kuhusu nyufa kwenye upande wa mbele wa nyumba yake; kuzuru shamba la Mlalamishi aliyelalamika kuhusu mitaro iliyojitengeneza katika shamba lake; na kuzuru nje ya eneo lililokuwa na ua ambalo lilikuwa na kisima kilichochimbwa wakati wa utafiti wa kijiolojia katika mwaka wa 2016;
- mikutano kwa njia ya simu na mikutano ya ana kwa ana na wanachama wa KVCO na wanachama wa JCAP;
- mkutano wa ana kwa ana na Wajumbe wawili wa Bunge la Kaunti ya Baringo, baada ya mapendekezo kutoka kwa Walalamishi;
- mkutano kwa njia ya simu na mkutano wa ana kwa ana na wawakilishi wa AOC mjini Nairobi;
- mikutano kwa njia ya simu na mikutano ya ana kwa ana na vikosi vya IFC vinavyoshughulikia AOC na Delonex; na
- mikutano kwa njia ya simu na mkutano wa ana kwa ana na wawakilishi wa Delonex mjini Iten, nchini Kenya.

Kwa kuwa baadhi ya malalamishi yaliyotolewa na Walalamishi yanahusu uauzi wa kijiolojia na uchimbaji wa visima uliofanywa na kampuni ya Tullow kati ya mwaka wa 2014 na mwaka wa 2016, kikosi cha CAO kilitafuta kampuni ya Tullow na kuipa fursa ya kutoa maoni yake. Kama tulivyoeleza hapo awali, Mradi huo wa Tullow haukufadhiliwa na IFC wala MIGA. Tullow ilitoa maoni yake wakati wa mkutano wa njia ya simu na kikosi cha CAO, na wakaomba kuwa maoni yao yajumuishwe katika ripoti ya tathmini (Tazama Kiambatisho A).

Ripoti hii inatoa muhtasari wa maoni yaliyosikilizwa na kikosi cha CAO kutoka kwa washikadau mbalimbali na inafafanua hatua zitakazofuatwa kwa kuzingatia uamuzi uliochukuliwa na Walalamishi, kampuni ya Delonex na kampuni ya Africa Oil.

### 3.2 Muhtasari wa Maoni

#### *3.2.1 Upande wa Walalamishi*

Kwa mjibu wa malalamishi, idadi ya Walalamishi ni wanajamii 140 kutoka kaunti za Baringo, Pokot Magharibi, na Elgeyo Marakwet. Katika malalamishi, kuna masuala kuhusiana na mchakato wa kushauriana na washikadau, kutokuwa na taarifa kuhusiana na Mradi, kutoshauriana na jamii zilizoathiriwa, na kutokuwepo na mfumo wa kutatua mizozo inayohusiana na Mradi huo.

Wakati wa ziara ya kufanya tathmini, kikosi cha CAO kilikutana na jumla ya Walalamishi 40 kutoka kwa jamii zifuatazo, waliojiwakilisha na/au walikuwa na kibali cha kuwakilisha jamii

zao: Salawa, Muchukwo, Barwessa, Arror, Tiaty, Kapluk, Kuikui, Kinyach, Katibel, Marigut, Kabutiei, Keturwo na Kaptilomo.

Kikundi kimoja cha Walalamishi (wanaotoka Kaskazini mwa Block 12A) walilalamika kuhusu utafiti wa kijiolojia uliotokea katika mwaka wa 2018 Kaskazini mwa Block hiyo, ili hali kikundi kingine cha Walalamishi (wanaotoka Kusini mwa Block 12A) walilalamika kuhusu utafiti wa kijiolojia uliotokea kati ya mwaka wa 2014 na mwaka wa 2016 Kusini mwa Block hiyo.

*a. Malalamishi kuhusiana na utafiti wa kijiolojia uliotokea mwaka wa 2018* Kaskazini mwa Block

Malalamishi yafuatayo ni masuala yanayohusiana na utafiti wa kijiolojia uliotokea katika mwaka wa 2018, wakati kampuni ya Delonex ilipochukua usukani wa uendeshaji wa mradi huo. Walalamishi walieleza kuwa utafiti huo wa kijiolojia ulijumuisha uauzi wa kijiolojia wanaolalamikia.

- ***Mchakato wa kushauriana na wadau:*** Baadhi ya Walalamishi walieleza kuwa, katika kijiji chao, kampuni ya Delonex ilishauriana tu na Chifu na wala wanajamii hawakushirikishwa moja kwa moja. Katika kijiji hicho, Walalamishi walieleza kuwa kampuni ya Delonex iliweka nyaya katika ardhi walionyeshwa na Chifu licha ya pingamizi kutoka kwa wanajamii. Kwa mjibu wa Walalamishi, hali hii ilisababisha mtafaruku na mzozo katika jamii. Walalamishi wengine walieleza kuwa maafisa wa uhusiano mwema na jamii (CLOs) wa kampuni ya Delonex hawazungumzi lugha ya eneo hilo na hivyo kukabiliwa na tatizo la kuwasilana moja kwa moja na wanajamii.

- ***Fidia ya matumizi ya ardhi kwa mda:*** Kuna baadhi ya Walalamishi walioeleza kuwa hawakuridhishwa na viwango vya fidia iliyotolewa na kampuni ya Delonex, ambavyo waliamini vilikuwa duni. Waliongezea kuwa wakati ambapo wamiliki wa ardhi walitoa malalamishi yao kuhusu viwango vya fidia, kampuni ya Delonex iliamua kutotumia mashamba yao badala ya kushauriana nao. Walalamishi wengine walieleza kuwa wakati ambapo maafisa wa uhusiano mwema na jamii (CLOs) wa kampuni ya Delonex walipokuja katika kijiji chao, waliwaeleza kuwa watalipa wamiliki wa ardhi fidia kupitia kwa Chifu. Ila, tangu wakati huo hakuna aliyepokea fidia yoyote. Waliongezea kuwa walioathirika zaidi kutokana na Mradi huo ni wajane, ambao mashamba yao yalinyakuliwa na watu walioamini kuwa ardhi hiyo itakuwa na thamani mno iwapo mafuta yangegunduliwa.

- ***Kazi ya uboreshaji wa ardhi na athari za uauzi wa kijiolojia kwa ardhi:*** Baadhi ya Walalamishi walidai kuwa kampuni ya Delonex haikuweka ahadi yake ya kuboresha ardhi yao na ya kuwa ardhi yao iliharibika kiwango cha kutoweza kuimarishwa. Walisema kuwa mitaro mikubwa kutokana na utafiti wa kijiolojia bado ipo.

- ***Usalama na matumizi ya maji:*** Kwa mjibu wa Walalamishi, milipuko iliyotokea wakati wa uauzi wa kijiolojia ilisababisha vumbi nyingi na kuogofya watu. Waliongezea kuwa wakati mwingine vilipuzi vilisahulika katika maeneo ya mradi na kuwa nyaya zilizowekwa zinaweza kupatwa na watoto, hali inayohatarisha maisha yao. Walalamishi pia walilamikia jinsi ambavyo kampuni ya Delonex ilivyotumia maji ya jamii ambayo hupatikana kwa nadra kuosha magari na mashine yao.

- ***Ajira kwa wenyeji:*** Walalamishi walitoa maoni kuwa kampuni ya Delonex haikutimiza ahadi iliyotoa ya kutoa kipaumbele kwa wenyeji wakati wa kutoa ajira. Baadhi ya Walalamishi walilamikia kutoridhishwa na hali ya kutoajiriwa kwao licha ya kuwa na tajriba (baadhi yao walifanya kazi na kampuni ya Tullow mbeleni, na wengine wao walihitimu kuwa wahandisi wa vifaa vya umeme), na kwamba wengi wa walioajiriwa hawakutoka

kwenye jamii zilizoathirika. Wengine wao walieleza kuwa ni Machifu tu ndiyo walioarifiwa kuhusu nafasi za kazi, na wala siyo jamii nzima kwa jumla na hivyo kupelekea machifu kuamua ni nani atakayeajiriwa. Wanadai kuwa nafasi hizi za kazi mara nyingi zilitolewa kwa watu kutoka kwa jamii ya machifu. Kwa kuongezea, Walalamishi walieleza kuwa ilikuwa nadra kwa kampuni ya Delonex kuajiri wanawake na eti, wafanyakazi wa kiume kwenye Mradi huu walijihusisha na mahusiano yalioenda kinyume cha maadili ya jamii, hali iliyosababisha mtafaruku na mizozo kwenye ndoa katika jamii.

- ***Mazingira ya kufanyia kazi:*** Walalamishi walihisi kuwa wenyeji wachache waliofanikiwa kuajiriwa, hasa baada ya malalamishi kutoka kwa wanajamii, walifanya kazi nyingi kwa ujira duni. Waliongezea kuwa iwapo wafanyikazi wangepata majeraha wakiwa kazini, hawakupata msaada wa kimatibabu kutoka kwa kampuni ya Delonex. Walisema kuwa kemikali zilizotumiwa na kampuni ya Delonex zilidhuru afya ya wafanyakazi, huku baadhi yao wakipata maambukizi kwenye mfumo wa kupumulia. Walalamishi wengi walieleza kuwa wanahofia kuathiriwa kiafya kwa kipindi cha mda mrefu.

b. *Malalamishi kuhusu utafiti wa kijiolojia uliotokea kati ya mwaka wa 2014 na mwaka wa 2016* Kusini mwa Block

Walalamishi walieleza kuwa utafiti wa kijiolojia, hasa uauzi wa kijiolojia na uchimbaji wa visima, ulifanyika katika mashamba yao kati ya mwaka wa 2014 na mwaka wa 2016, wakati Mradi huo ulipoendeshwa na kampuni ya Tullow.

- ***Mchakato wa kushauriana na washikadau:*** Walalamishi walieleza kuwa wamiliki na waendeshaji wa mradi (wakati huo, kampuni ya Tullow) walishauriana tu na wawakilishi wa serikali, hasa Machifu (ambao ni wafanyakazi wa serikali ya taifa) na wala hawakushauriana na wanajamii wala viongozi wao. Walalamishi wanaamini kuwa wana haki ya kuelezwa kuhusu miradi ili wafahamu kuhusu manufaa na madhara ya miradi hiyo kwa ardhi yao. Pia, walisema kuwa serikali ingeshauriana nao kabla ya kuruhusu mtu yeyote kuendesha shughuli kwa Block 12A. Walisema kuwa ESIA iliandaliwa na kuchapishwa bila kushauriana na wanajamii (walidai kuwa walitoa malalamishi kwa Mamlaka ya Kitaifa ya Usimamizi wa Mazingira (NEMA) kuhusu suala hili bila mafanikio. Walalamishi pia walielezea kuwa haikuwa rahisi kupata Tathmini ya Athari kwa Mazingira na kwa Jamii (ESIA) na wanadai kuwa hawakupata fursa ya kushughulikia kauli zilizoko katika ESIA au kutoa maoni yao. Walishangaa kuona magari yakija kwenye mashamba yao bila kufahamu kilichokuwa kinaendelea na wakasema kuwa hawengetamini kukumbwa na hali kama hiyo tena. Baadhi ya Walalamishi walisema kuwa mwendeshaji wa mradi alikuja kwenye jamii zao na hata kujaribu kuwahonga kupitia zawadi. Walieleza kuwa wakati walipokataa kuchukua zawadi na kuhamasisha wanajamii ili wapate taarifa zaidi kuhusiana na mradi huo, waliambiwa kuwa mradi huo ungehamishiwa kwengineko nchini. Walalamishi walisema kuwa wale waliolalamika au kuuliza maswali kuhusiana na mradi walirejelewa kama "wapinga maendeleo" na hivyo kubaguliwa.

  KVCO ilielezea CAO kuwa, baada ya kuiandikia mara kadhaa, kampuni ya Tullow iliwaandikia ikiahidi kuwa itaboresha mawasiliano na wanajamii na kuwaruhusu kutoa malalamishi yao huku wakiahidi kuyashughulikia upesi. Hata hivyo, KVCO ilidai kuwa hawakuweka ahadi hiyo. Walalamishi walisema kuwa hakukuwepo na mfumo wa kutatua mizozo katika Block 12A. Pia waliongezea kuwa, wakati wa mkutano na jamii uliotokea kati ya mwezi wa Septemba na mwezi wa Octoba mwaka wa 2014, wanajamii waliomba kupata taarifa moja kwa moja na wala sio kupitia kwa maafisa wa serikali, lakini ombi lao halikuzingatiwa. KVCO pia ilisema kuwa wanajamii walishirikishwa kupitia jukwaa la shirika la uraia ila KVCO haikuruhusiwa kushiriki.

Kwa kuongezea, Walalamishi walisema walihisi kuwa mwendeshaji wa mradi alikuwa na uhusiano wa karibu na serikali kwa sababu mara kwa mara wafanyakazi wa serikali walionekana wakiwa wamevalia mashati yaliyo na nembo ya kampuni. Kwa mfano, wakati ambapo wenyeji walihitaji kuajiriwa kwenye mradi huo, Walalamishi walisema Machifu waliambiwa na wangeamua ni nani atakayeajiriwa - hasa watu kutoka jamii ya Machifu hao. Walalamishi pia walidai kuwa mwendeshaji wa mradi ana ushawishi mkubwa kwa maafisa wa serikali, ambao kila mara huwa upande wao. Walalamishi pia walidai kuwa baadhi wa Machifu walikubali hongo, na kuwa mmoja wa Machifu hao alikodisha shule ya jamii pasipo na ruhusa kutoka kwa jamii.

- ***Upatikanaji wa ardhi:*** Kuna baadhi ya Walalamishi waliodai kuwa wakati wa utafiti wa kijiolojia, uliofanyika kati ya mwaka wa 2014 na mwaka wa 2016, mashamba yao yalitumiwa bila ruhusa yao na masuala ya jinsi ya kuchukua ardhi na jinsi ya kulipa fidia yalijadiliwa na Chifu wa mtaa badala ya kushauriana na wamiliki wa ardhi moja kwa moja. Waliezea kuwa wakati wowote kampuni ya Tullow ilipoenda kwenye ardhi yao, waliandama na Machifu wakati wote. Na iwapo wenye mashamba wangepinga, Machifu walijaribu kuwanyamazisha kwa kusema kuwa ilikuwa "kazi ya serikali" na wanapaswa kutowazuia kufanya kazi yao. Baadhi yao walisema kuwa walipewa vitisho vya kufungwa au kuitiwa polisi iwapo hawangeruhusu kampuni ya Tullow kwenye mashamba yao.

- ***Fidia kwa kutumia ardhi kwa mda:*** Walalamishi walieleza kuwa hawakuelewa ni kwa nini viwango vinavyotofautiana vya fidia vilitumiwa katika kaunti mbalimbali ili kupata ardhi. Walidai kuwa viwango vya fidia vilikuwa duni na visivyofaa. Walalamishi walieleza kuwa wamiliki wa ardhi walitakiwa kutoeleza wenzao wakati walipopokea fidia yao.

- ***Kazi ya uboreshaji wa ardhi na athari za uauzi wa kijiolojia kwa ardhi, kwa majengo na kwa maeneo matakatifu:*** Walalamishi walieleza kuwa utafiti wa kijiolojia ulisababisha mmomonyoko wa udongo na kuwa mashamba yao hayakuboreshwa ipasavyo. Walisema kuwa mitaro mikubwa ilijitokeza katika mashamba yao baada ya utafiti wa kijiolojia. Hali hii ilifanya kuwa vigumu kuotesha mimea, kuchunga mifugo, au hata kutembea shambani. Walalamishi waliamini kuwa mitaro hiyo ilitokana na uauzi wa kijiolojia na matumizi ya vilipuzi. Kuna baadhi ya Walalamishi waliolalamika kuwa mashamba yao yaliyokuwa na rutuba hapo awali, hayangeweza kutumika baada ya utafiti wa kijiolojia kutokana na hali ya kutoziba mitaro iliyochimbwa au ilizibwa kwa kutumia mawe na magogo badala ya mchanga. Walalamishi waliongezea kuwa hawakupokea fidia yoyote ya kufidia uharibifu wa aina hii kwa mashamba yao. Kuna baadhi ya Walalamishi waliosema kuwa vilipuzi vilivyoachwa nyuma vilikuwa hatari, hasa kwa watoto kutoka eneo hilo. Pia, walisikitishwa kwa kutofidiwa, au kwa kupokea fidia duni, wakati nyua zao zilipoharibiwa hasa za mimea, ikijumuisha miti midogomidogo au vichaka vinavyowekwa kuashiria mipaka ya shamba. Pia walisema kuwa nyua zao hazikurudishwa jinsi zilivyokuwa hapo awali.

  Kwa kuongezea, Walalamishi walielezea kuwa, kuna wakati walipoona nyufa kwenye nyumba zao. Walisema nyufa hizo zilisababishwa na uauzi wa kijiolojia uliofanywa. Wengine wao walikuwa na maoni kuwa uauzi wa kijiolojia ulifanywa karibu mno na nyumba zao, hali wanayoamini ndiyo iliyosababisha nyufa kwa nyumba zao. Wengine wao walielezea kuwa walisisitiza walihitaji kufidiwa kutokana na madhara yaliyotokea kwa nyumba zao. Badala yake, walipokea vitisho na kuambiwa wasifuatilie masuala hayo kwa sababu mwendeshaji wa mradi huo ilikuwa kampuni kubwa na maarufu.

  Walalamishi waliongezea kuwa utafiti wa kijiolojia ulisababisha uharibifu wa maeneo mengi matakatifu, ikiwa ni pamoja na miti mitakatifu na maeneo yanayotumiwa na jamii kufanyia ibada.

- ***Athari kwa maji na kwa afya:*** Walalamishi walidai kuwa matumizi ya kemikali wakati wa utafiti wa kijiolojia yalisababisha uchafuzi wa maji. Kwa mjibu wa Walalamishi, baada ya utafiti wa kijiolojia kufanyika, watu walianza kuwa wagonjwa walipotumia maji hayo. Hali hii ilisababisha jamii kipindi fulani kuacha kutumia maji hayo. Waliongezea kuwa hata mifugo wao walipata ugonjwa wa ngozi walipotumia maji hayo. Walalamishi pia walieleza kuwa utafiti wa kijiolojia ulisababisha maeneo yenye ouevu kudidimia. Kwa kuongezea, walieleza kuwa nyuki waliokuwa wamefugwa ili kupata asali walihama kutokana na utafiti wa kijiolojia. Baadhi ya Walalamishi walielezea kuwa wakati wa utafiti wa kijiolojia, hasa baada ya kuchimba kisima, walishangaa kuona idadi kubwa ya wanyama waliokuwa na mimba wakipoteza ujaa uzito na/au wakifa.

- ***Ajira kwa wenyeji na mazingira ya kufanyia kazi:*** Walalamishi walieleza kuwa ni wenyeji wachache mno walioajiriwa kufanya kazi kwa Block 12A, hasa kufanya kazi zisizohitaji mafunzo maalum, kama madereva na wajakazi. Kwa mjibu wa Walalamishi, wafanyakazi walifanya kazi nyingi kwa ujira duni.

- **Madai ya unyanyasaji wa kijinsia:** Baadhi ya Walalamishi walielezea kikosi cha CAO matukio yaliashiria kuwa kulitokea mashambulizi ya kimapenzi, unyanyasaji wa kimapenzi na unyanyasaji mwingine wa kijinsia uliofanywa na wafanyakazi walioshiriki kwenye utafiti wa kijiolojia kwenye Block 12A. Matukio hayo, kwa mjibu wa Walalamishi, yalihusisha wanawake na wasichana. Katika baadha ya jamii, hali hii ilisababisha mtafaruku katika jamii. Hakuna malalamisi rasmi au tukio rasmi lililoripotiwa au hata lililorejelewa wakati wa tathmini iliyofanywa na CAO.

- ***Programu za kuonyesha uwajibikaji wa shirika:*** Walalamishi walisema ya kwamba walisikia kuwa kampuni ya Tullow ilifadhili watu kusoma, ila wao na wanajamii wenzao hawakunufaika na ufadhili huo. Wanaamini kuwa wale waliofadhiliwa sio wale walioathiriwa moja kwa moja kutokana na utafiti wa kijiolojia.

- ***Haki ya kupata mali ghafi na kugawana faida:*** Walalamishi walilalamika kuhusu hali ya baadaye na wangependa kujua jinsi hali itakavyokuwa iwapo mafuta yangepatikana. Je mafuta hayo yatakuwa ya nani? Ni nini kitakachofanyika katika mashamba yao? Hawajui iwapo jamii itanufaika iwapo mafuta yatapatikana. Baadhi ya Walalamishi walieleza kuwa waliamini kwamba asilimia fulani ya faida kutoka kwa Mradi huo ilipaswa kuwa ya wanajamii.

- ***Hati ya kumiliki ardhi:*** Walalamishi pia walielezea athari ya mradi huo kwa umiliki wa ardhi. Walielezea kuwa ni watu wachache tu katika eneo hilo wanaomiliki hati ya kumiliki ardhi na utafiti wa kijiolojia unaweza kuongeza bei ya shamba na hivyo kupelekea unyakuzi wa ardhi.

### *3.2.2 Upande wa kampuni ya Delonex*

Kampuni ya Delonex ilisema kuwa ijapokuwa ilikuwa na nia ya kushiriki kwenye Mradi katika Block 12A mwezi wa Septemba mwaka wa 2015, kampuni ya Tullow ilikuwa mwendeshaji wa mradi na mmliki mkuu wa Block 12A hadi mwezi wa Januari mwaka wa 2018. Waliongezea kuwa hawakufahamu kuwa kulikuwepo na utafiti wa kijiolojia nyanjani kati ya mwezi wa April mwaka wa 2016 na mwezi wa Mechi mwaka wa 2018. Mnamo Januari mwaka wa 2018, Kampuni ya Delonex ilichukua usukani wa kuendesha mradi. Wakati huo,

Delonex ilibaini kuwa data zaidi zilihitajika na hivyo ikaamua kufanya uauzi wa kijiolojia katika Block 12A, katika eneo linalopita ndani ya kaunti tatu: Baringo (hasa Baringo Kusini na Tiati), Elgeyo-Marakwet (hasa Marakwet Magharibi na Mashariki) na Pokot Magharibi (hasa Sigor). Kampuni ya Delonex pia ilisema kuwa mradi wao haukupita katika jamii za Barwesa na Muchukwo zinazotajwa katika malalamishi. Delonex ilihudumu katika maeneo matatu: Marigut, Ayatia na Kuikui. Delonex iliambia CAO maeneo waliofanya uauzi wa kijiolojia ni tofauti na yale Tullow ilifanyia kati ya mwaka wa 2013 na mwaka wa 2014. Shughuli za uauzi wa kijiolojia na za uchimbaji wa visima zilizofanywa na kampuni ya Tullow zilitokea kusini mwa Block 12A katika eneo la Kerio Valley.

Kwa mjibu wa Delonex, uauzi wa kijiolojia unamaanisha kufanya utafiti wa kijuujuu ili kuelewa mfumo wa chini ya ardhi na kubainisha maeneo ambayo haidrokabani zinapatikana. Inajumuisha kutuma vitetemeshi ardhini na kisha kurekodi hali inayoonekena. Vitetemeshi vivyo hutoka kwa magari ya vitetemeshi au kwa vilipuzi vinavyowekwa katika mashimo ya mita 12 ardhini. Delonex iliongeza kuwa wakati wa uauzi wa kijiolojia, nyaya zilizo na maikrofoni za kurekodi mitetemeko ya kijiolojia huwekwa ardhini ili kurekodi mitetemeko inayosababishwa na magari au vilipuzi. Ili kuweka nyaya hizo ili kufanya utafiti, ni sharti mimea iondolewe ili kuweka mitaro ya kuingiza nyaya na kuwezesha wanaofanya kazi kuzifikia. Data inayokusanywa hutumwa kwa wataalamu kuzichunguza na kuzichanganua.

Hapa, Delonex ilieleza kuwa walifanya uauzi wa kijiolojia kaskazini mwa Block 12A kuanzia mwezi wa Aprili hadi mwezi wa Oktoba mwaka wa 2018. Wakati wa kufanya uauzi wa kijiolojia, Delonex ilitoa kandarasi na kufanya kazi na kikosi cha wataalamu kwa jina la BGP. Delonex ilieleza kuwa hawajafanya utafiti mwingine wowote wa kijiolojia tangu mwezi wa Oktoba mwaka wa 2018. Walieleza kuwa bado walikuwa wanachanganua data iliyokusanywa mwaka wa 2018 na kuwa matokeo ya utafiti huo ndiyo yatakayoamua iwapo wataendelea na shughuli katika Block 12A.

Delonex pia ilieleza kuwa, walijadiliana na Tullow ili kujifunza kutokana na tajriba yao kama waendeshaji wa mradi katika Block 12A ili wanufaike kutokana na maoni yao. Kwa mfano, Delonex waliuliza mtaalamu kupitia viwango vya fidia vilivyotumika Baringo, Elgeyo-Marakwet na Pokot Magharibi. Delonex ilisema kuwa walihakikisha kwamba walishirikiana na viongozi wa jamii kwa sababu waliamini kuwa wanaaminiwa na jamii zao. Delonex ilieleza kuwa kushirikiana kwao na Machifu kulikuwa muhimu, kwa sababu wanawakilisha serikali na wana kibali cha kuhamasisha na kuandaa mikutano ya jamii nyanjani.

- ***Mchakato wa kushauriana na washikadau:*** Delonex ilisema kuwa iliajiri maafisa watatu wa uhusiano mwema na jamii (CLOs), Meneja wa Washikadau Nyanjani/Msimamizi wa Jamii, aliyejadiliana mara kwa mara na jamii, na machifu wa kata, na wazee kuhusiana na shughuli za Delonex.

  Delonex ilisema kuwa waliandaa mikutano rasmi ya uhamasishaji katika kaunti kabla ya mradi mnamo Mechi mwaka wa 2018: mmoja Baringo, mwingine Elgeyo-Marakwet na mwingine Pokot Magharibi. Walisema kuwa baada ya mikutano hiyo, kikosi chao kiliandaa mikutano ya umma na jamii ambazo shughuli za mradi huo zingefanyika moja kwa moja, ili kuwaelezea na kuwapa taarifa na kujibu maswali (shughuli za aina hii zilifika 144). Walisema kuwa pia walikuwa na mikutano isiyo rasmi kwa sababu kikosi chao kilikuwa nyanjani usiku na mchana, kila siku za juma kati ya mwezi wa Mechi na wa Oktoba mwaka wa 2018. Kwa mjibu wa kampuni, wakati mwingine ilipohitajika, walitumia lugha za wenyeji kuwasiliana.

  Delonex iliongeza kuwa, walipofanya utafiti ili kuamua maeneo ya kuweka nyaya, walijadiliana na wazee na wanajamii, na wakapewa fursa ya kutoa maoni yao kuhusu maeneo ya kuweka nyaya. Kwa mfano, Delonex ilisema walitambua kuna maeneo yanayothaminiwa na muhimu kwa utamaduni ili kujizuia kuyafanyia madhara. Kwa

kuongezea, pale ambapo wamiliki wa mashamba walikataa wasipitishie nyaya mashambani mwao, Delonex ilitafuta njia mbadala.

- ***Upatikanaji wa ardhi:*** Delonex ilieleza kuwa kabla ya kupitia kwenye ardhi yoyote, waliomba ruhusa ya kuitumia kwa mda kutoka kwa mmiliki/mtumiaji wa ardhi hiyo. Katika maeneo ambayo hakukuwepo na hati ya umiliki (hali iliyotokea mara kwa mara katika maeneo ya uauzi wa kijiolojia), kampuni iliomba ruhusa kutoka kwa aliyekuwa anatumia ardhi hiyo. Wazee wa mtaa kutoka katika jamii walisaidia kutambulisha mmiliki au mtumiaji wa ardhi iliyotumika katika uauzi wa kijiolojia. Mtumiaji wa ardhi hiyo alipokea hadhi sawa na wale waliomiliki hati miliki ya ardhi. Kwa mjibu wa Delonex, ruhusa ya kutumia shamba kwa mda ilithibitishwa kupitia kwa kutia sahihi na mmiliki au mtumiaji wa ardhi kwa fomu ya kukubali kutoa Kibali cha Matumizi kwa Mda (PTA). Hakuna ardhi iliyochukuliwa na ardhi yoyote iliyotumiwa ilitumika tu kwa mda. Hakuna uhamaji uliohitajika wakati wa mradi.

- ***Fidia ya matumizi ya ardhi kwa mda:*** Delonex ilisema kuwa ililipa wamiliki/watumiaji wa ardhi fidia kwa kupoteza mimea yao na kwa usumbufu, huku asilimia 15 ya thamani ya mimea ikijumuishwa kama gharama ya usumbufu. Delonex iliongezea kuwa viwango vyao vya fidia vilipitiwa na wataalamu, na vilikuwa vya juu ikilinganishwa na vile vilivyotolewa na kampuni ya Tullow. Pia waliamua kutumia viwango vinavyofanana katika kaunti zote tatu. Delonex ilisema kuwa pia ilijumuisha viwango vya fidia ya mimea ya majani iliyopandwa na mishubiri, hali ambayo haikushuhuduwa awali. Kwa mjibu wa Delonex, serikali za kaunti na jamii zilifurahi kwa sababu viwango sawa vilitumika na vilikuwa bora kuliko vilivyotumika hapo awali.

- ***Kazi ya uboreshaji wa ardhi na athari za uauzi wa kijiolojia kwa ardhi:*** Delonex ilieleza kuwa baada ya utafiti kukamilika na nyaya kuondolewa, waliboresha mashamba yote kulingana na kile kilichohitajika, na kuridhisha kila mmiliki/mtumiaji wa ardhi zote zilizotumika wakati wa uboreshaji. Baada ya kuboreshwa, kila mimiliki/mtumiaji wa ardhi alitia sahihi stakabadhi zilizoonyesha kuwa waliridhishwa na hali ya ardhi iliyorudishwa (inayoitwa fomu ya kuondoa kibali). Delonex iliongeza kuwa eneo hilo hukumbwa na mmonyoko wa udongo na kuwa ukataji wa miti ambao hutokea ili kuchoma makaa unaofanywa mara kwa mara na wanajamii huchangia hali hii kuwa mbaya zaidi.

  Delonex ilisema kuwa vilipuzi walivyotumia huyeyuka na iwapo havikulipuka vingeyeyuka vyenyewe. Kwa mjibu wa Delonex, matumizi ya vilipuzi huongozwa na sheria kali nchini Kenya na kuwa kazi yao ilifuatiliwa kwa karibu na Wizara ya Uchimbaji wa Madini. Walieleza kuwa pia kuwa wanajamii walielezwa kuhusu utaratibu utakaotumika katika zoezi hilo wakati wa mchakato wa majadiliano na washikadau.

  Delonex ilidai kuwa ilipokea malalamishi kutoka kwa serikali kuu au kutoka kwa shirika linalosimamia sheria kuhusiana na miradi ya utafiti wa mafuta na gesi au hata NEMA, Mamlaka ya Kitaifa Inayosimamia Mazingira, taasisi ya serikali ya Kenya inayosimamia ushughulikiaji wa mazingira, na sera za mazingira. Waliongezea kuwa wakati wa mradi au baada ya mradi, hawakupokea malalamishi yoyote kutoka kwa KVCO. Delonex iliongeza pia kuwa walipokea malamishi saba kupitia mfumo wao wa kutatua mizozo, na kuwa ni lalamishi moja tu ambalo halingeweza kushughulikiwa kiwango cha kumridhisha mlalamishi. Kwa mjibu wa Delonex, hii ni kwa sababu mlalamishi alikuwa anaitisha fidia ya mimea, ili hali mimea yoyote haikuwepo na kwa hivyo hakuna fidia ilihitajika.

  Delonex ilisema kuwa kama desturi yao, miti iliyo na upana wa sentimita 20 haipaswi kukatwa, na wakikumbuka vizuri, hawakuharibu miti yoyote mipana zaidi wakati wa uauzi wa kijiolojia. Kwa mjibu wa Delonex, njia za nyaya kupitia wakati wa uauzi wa kijiolojia zilibadilishwa iwapo zingepitia katika maeneo matakatifu, maeneo yaliyo na miti iliyo na upana wa sentimita zaidi ya 20, majengo na makaburi.

- ***Ajira kwa wenyeji:*** Delonex ilisema kuwa wenyeji 182 waliajiriwa wakati wa uauzi wa kijiolojia, ikijumuisha wafanyikazi wa mda. Hawakupokea malalamishi yoyote kuhusiana na ajira. Delonex ilisema kuwa kipaumbele kilitolewa kwa jamii zilizoathiriwa zaidi na shughuli za mradi na kuwa kampuni iliyopewa kandarasi ya BGP, iliweka mabango katika maeneo mbalimbali yaliathiriwa ili kuhakikisha kuwa kila mtu anafahamu kuhusu nafasi za kazi zilizotangazwa. Kwa mjibu wa Delonex, watu waliofanya kazi katika mradi huu waliishi na kununua chakula kutoka kwa wenyeji, hali iliyoimaisha biashara na kuongezea wenyeji kipato katika maeneo husika.

- ***Programu za Kuonyesha Uwajibikaji wa Shirika (CSR):*** Delonex ilisema kuwa serikali iliwauliza kutoa msaada ili kuhakikisha amani inadumu na kuimarisha uhusiano kati ya makabila mbalimbali katika eneo hilo, eneo lililoshuhudia mizozo na ghasia za kikabila hata kabla ya mradi huu na wakati wa mradi huu. Walisema kuwa, kwa mfano, wao kuajiri watu kutoka katika kaunti zote tatu, wanaotoka katika makabila mbalimbali, ili wafanye kazi pamoja kwa umoja, ni kipengele mojawapo cha mradi huu. Delonex ilitii ombi hili na wakati wa kazi mizozo yoyote ya kikabila haikushuhudiwa kati ya wafanyakazi.

  Kwa kuongezea, Delonex ilisema kuwa walitoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi 509 kutoka eneo hilo na kuwajengea uwezo kupitia programu ya mafunzo kuhusu kilimo, mafunzo yaliyotolewa kwa watu 80 katika jamii husika.

Kwa jumla, kampuni hiyo ilieleza kuwa ilikuwa tayari kushiriki katika majidiliano muhimu na wanajamii.

#### *3.2.3 Upande wa AOC*

AOC ilieleza kuwa ijapokuwa hapo awali walimiliki hisa kwa Block 12A tangu mwaka wa 2010 hadi mwaka wa 2017, hawakuwahi kuendesha mradi huo na ya kuwa Tullow iliendesha mradi huo kipindi hicho. AOC iliongeza kuwa ilijiondoa kwenye mradi huo mwaka wa 2017 (ijapokuwa wao bado ni mteja wa IFC). Kutokana na sababu hizi, AOC ilisema hawangeweza kusema chochote kuhusu malalamishi yaliyotolewa. Waliongezea kuwa waliamini Tullow na Delonex (Delonex ilianza kufanya kazi baada ya kuondoka kwa AOC) walifuata Kanuni za Utendakazi za IFC.

## 4. HATUA ZINAZOFUATA

Wakati wa mchakato wa tathmini iliyofanywa na CAO, Walalamishi na kampuni ya Delonex walionyesha walitaka kushughulikia masuala yaliyoibuliwa katika malalamishi kupitia mchakato wa majadiliano ya hiari yanayoendeshwa na kitengo cha CAO cha Kutatua Mizozo. Mchakato huo utaendeshwa na CAO, ikiwa ni pamoja na kusaidia wahusika kujiandaa kwa mawasiliano, kukubaliana kuhusu kanuni zitakazotumika na yale yatakayojumuishwa katika majadiliano na kushirikiana kutafuta suluhu la malalamishi yaliyotolewa kwa muhtasari katika ripoti hii. AOC haitashiriki katika mchakato huu, kama ilivyoelezwa hapo awali. Tullow ilieleza CAO kuwa wanaweza kushiriki katika majadiliano hayo, hasa kama mwangalizi, iwapo wahusika wataelewana kuhusu utaratibu watakaotumiwa.

**KIAMBATISHO A. MAONI YA TULLOW**

Tullow si mteja wa IFC kuhusiana na mradi huu na haitashiriki katika mchakato wa CAO. Hata hivyo, kama sehemu ya tathmini, CAO hujadiliana na washikadau inapopokea mapendekezo kutoka kwa wahusika yanayoweza kuimairisha uelewa wa CAO kuhusu hali iliopo. Katika muktadha huu, CAO ilizungumza na Tullow, iliyowaeleza kuwa walianza kuendesha shughuli kwenye Block 12A katika mwaka wa 2011 baada ya kutia sahihi Makubaliano ya Kuendesha Mradi Pamoja na kampuni ya Africa Oil. Tullow iliongeza kuwa kati ya mwaka wa 2011 na mwaka wa 2018 (walipoacha kuendesha mradi), walifanya utafiti wa kijiolojia kwenye Block 12A kwa kipindi cha miaka miwili, kati ya mwaka wa 2014 na mwaka wa 2016. Tullow walikuwa tayari kutoa maoni yao kuhusiana na malalamishi kuhusu athari za utafiti wa kijiolojia kati ya mwaka wa 2014 na mwaka wa 2016, walisema ulihusisha uauzi wa kijiolojia, unaofanywa kwa kuweka nyaya ardhini ili kurekodi mitetemeko inayosababishwa na magari au vilipuzi vidogo.

- ***Mchakato wa kushauriana na washikadau:*** Kampuni ya Tullow ilisema kuwa kabla ya kuanza uauzi wa kijiolojia, walifanya ESIA na kushauriana kwa kina na washikadau, ikiwa ni pamoja na serikali, NGO zinazopatikana maeneo hayo, Machifu wa jamii, na wanajamii ambao wangeathiriwa kutokana na shughuli za uauzi wa kijiolojia. Tullow ilieleza kuwa waliajiri watu waliotumia lugha za wenyeji ili kushirikisha wanajamii. Pia walichapisha vipeperushi na kuvisambaza, ijapokuwa vilikuwa katika Kiingereza na Kiswahili ambazo ni lugha za kitaifa nchini Kenya.

  Tullow ilisema walianza kwa kuorodhesha washikadau, kipindi ambacho pia walikutana na Magavana wa Kaunti za Baringo na Elgeyo-Marakwet. Pia, walikutana na Machifu na jamii kwa jumla ili kuwaelezea lengo la mradi. Tullow ilieleza kuwa mikutano ya umma ilikuwa wazi kwa yeyote aliyetaka kuhudhuhuria. Mikutano hiyo ilifanyika kwa Chifu, au mahali maalumu nje, au wakati mwingine shuleni eneo hilo.

  Kuhusiana na upatikanaji wa taarifa, Tullow ilisema kuwa ESIA yao inapatikana kwa umma kupitia tovuti yao na iliwekwa wazi mtandaoni mwanzoni wa mradi. Tullow iliongezea kuwa walichapisha na kutoa makala ya ESIA kwa Afisi za Gavana wa Kaunti na NEMA katika Kaunti za Baringo na Elgeyo-Marakwet ili kuwezesha watu wasiotumia mtandao kuyasoma. Kwa kuongezea, Tullow ilieleza kuwa walitoa taarifa zilizohitajika kwa kuzungumza na wanajamii wakati wa mikutano kadhaa waliofanya nao.

  Tullow ilieleza kuwa maafisa wao wa uhusiano mwema na jamii walikuwa katika eneo la mradi kabla ya kuanza uauzi wa kijiolojia na waliondoka miaka miwili baada ya utafiti kuhitimika. Kipindi hicho, maafisa wa uhusiano mwema na jamii walikuwa tayari kujibu masuali mda huo wote. Kwa kuongezea, maafisa wa uhusiano mwema na jamii walijadiliana na wanajamii na hata kufanya mikutano nao, kwa mfano kwenye maeneo ya kuteka maji, maeneo wanayopenda kukusanyika. Maafisa wa uhusiano mwema na jamii pia walishiriki katika mikutano ya jamii. Kwa jumla, Tullow ilieleza kuwa maafisa wa uhusiano mwema mara nyingi walipatikana katika jamii.

- ***Upatikanaji wa ardhi:*** Wakati wa kuorodhesha washikadau, Tullow iligundua kuwa watumiajii wengi wa ardhi hawakuwa na hati miliki ya ardhi. Ili kubainisha mumiliki wa ardhi, walifanya utafiti wa maeneo walionuia kuweka nyaya za uauzi wa kijiolojia. Waliandamana na wazee waliwawezesha kubainisha watumiaji wa ardhi, na kuwatambulisha kwa wamiliki wa ardhi. Wazee hao waliwaelezea mahali shule, mito na maeneo matakatifu yalipopatikana. Tullow pia ilieleza kuwa walibadilisha njia nyingi za kufuatwa na nyaya kwa kuzingatia haya na pale ambapo watumiaji wa ardhi walipinga shughuli za uauzi wa kujiolojia kutokea kwenye mashamba yao. Tullow ilielezea kuwa baadaye waliandaa mikutano na watumiaji wote wa ardhi ili kupitia na kudhibitisha taarifa walizopokea kutoka kwa wazee. Kwa mjibu wa Tullow, walikutana na kila mmiliki wa

ardhi na mtumiaji wa ardhi ili kuruhusu Tullow kuweka nyaya kwa mda katika ardhi yao. Tullow aliwaelezea lengo la uauzi na jinsi uauzi wa kujiolojia hufanywa, pamoja na ukweli kuwa uauzi wa kujiolojia ungefanywa tu kwa mda. Tullow ilieleza kuwa kila mmiliki wa ardhi alikuwa na uhuru wa kuamua kuwaruhusu au kuwapinga kutumia ardhi yao au kupitia kwa mashamba yao. Waliokubali walitia sahihi fomu kuwaruhu kutumia ardhi yao.

- ***Fidia ya kutumia ardhi kwa mda:*** Kampuni ya Tullow ilieleza kuwa iliajiri washauri wa kuwasaidia kubainisha viwango mwafaka vya kulipa kama fidia kwa kutumia ardhi kwa mda na hasara ya mimea. Kwa kuwa kipindi hicho hakukuwepo na mfumo wa kuwaongoza nchini Kenya, Tullow ilieleza kuwa walijadilina kuhusu fidia kwa kuzingatia viwango vinavyotumika katika Kaunti wakati wa kukodisha ardhi. Kwa kuongezea, Tullow ilieleza kuwa walitoa fidia ya kufidia hasara ya mimea kwa kuzingatia aina ya mmea kwenye shamba. Tullow ilisisitiza kuwa walifidia tu wamiliki wa ardhi na watumiaji wa ardhi ambao mashamba yao yalitumika kwa uauzi wa kijiolojia.

- ***Kazi ya uboreshaji wa ardhi na athari za uauzi wa kijiolojia kwa ardhi,*** Kampuni ya Tullow ilieleza kuwa baada ya kukamilisha uauzi wa kijiolojia, Tullow iliondoa nyaya zake na kutumia watu wanaojitegemea kutathmini uwezekano wa madhara kwa ardhi na kupanga kufanya kazi ya uboreshaji. Kwa mjibu wa Tullow, ardhi ya Block 12A ni ngumu mno hali inayopelekea mmomonyoko wa udongo, kutokana na kulisha mifugo na uchomaji wa makaa. Tullow inaamini kuwa masuala haya mawili ndiyo sababu kuu za mmomonyoko wa udongo, na wala siyo utafiti wa kijiolojia. Hata hivyo, bila kuzingatia chanzo cha mmomonyoko wa udongo, Tullow ilisema kuwa mbinu yao kila mara ilikuwa ni kujaribu kusaidia wanajamii kupata suluhu ya kudumu. Kwa kuzingatia haya, walisema kuwa walijidaliana na wamiliki wa ardhi ili kujadili kuhusu uboreshaji wa kudumu. Kwa mfano walipendekeza upandaji wa miti inayokita mizizi zaidi. Baadhi ya wamiliki wa ardhi walikubali, ila kuna wale waliopendelea kutumia mbinu zisizoweza kudumu. Kwa mjibu wa Tullow, kuna baadhi ya watu ambao hawakuridhishwa wakati kampuni ya Tullow ilipokataa kuwapa fedha kama fidia kutokana na athari za utafiti huo kwenye ardhi yao.

  Tullow ilielezea CAO kuwa walitia sahihi Mkataba wa Makubaliano (MOU) na Serikali ya Kaunti ambapo wao wangeboresha ardhi hiyo halafu kampuni ya Tullow ingelipia. Tullow ilieleza kuwa hakakudhibitisha iwapo wamiliki wote wa ardhi waliridhishwa na kazi ya uboreshaji wa ardhi.

- ***Ajira kwa wenyeji:*** Kampuni ya Tullow ilieleza kuwa walitoa kandarasi ya kufanya uauzi wa kijiolojia kwa kampuni kwa jina la BGP. Ijapokuwa Tullow iliendeleza huo mradi, kampuni ya BGP ndiyo iliyoendeleza uauzi wa kijiolojia na kuajiri wanajamii wakati wa uauzi huo wa kijiolojia. Kampuni ya Tullow ilieleza kuwa walikutana na Machifu wa jamii kuwafahamisha kuhusu nafasi hizo za kazi. Matangazo ya nafasi ya kazi pia yaliwekwa kwa afisi za Machifu na kwenye maeneo ya kuwekewa matangazo vitongojini. Fursa ya kwanza ya ajira ilikuwa ujenzi wa kampi mbili za uauzi wa kijiolojia kwa mda wa miezi miwili. Tullow ilieleza kuwa kampuni ya BGP ilielezea wanakijiji wazi walipoajiriwa katika eneo la ujenzi kuwa kazi hiyo ilikuwa tu ya mda na itahusisha tu ujenzi wa kampi. Hata hivyo, wafanyakazi wengi hawakuridhishwa kuwa kampuni ya BGP haingewaajiri baada ya hapo. Baadaye, kampuni ya BGP iliajiri wanajamii kuweka nyaya. Kipaumbele kilitolewa kwa watu kutoka kwa jamii zilizoishi karibu na maeneo yaliyowekwa nyaya.

  Kuhusiana na madai ya unyanyasaji wa kijinsia, Tullow walisema kuwa hawakuwahi kupokea malalamishi yoyote kuhusiana na hali hiyo, na iwapo wangeyapokea wangeyashughulikia ipasavyo. Tullow iliongezea kuwa kabla ya kuajiri kampuni ya BGP, walikuwa wamefanya utafiti na kuridhishwa nao. Tullow ilieleza kuwa kandarasi kati ya kampuni ya Tullow na kampuni ya BGP ililazimu BGP na wafanyakazi kufuata Maadili ya Utendakazi ya Tullow.

- ***Programu za kuonyesha uwajibikaji wa shirika:*** Kampuni ya Tullow ilisema kuwa walifadhili miradi ya maji na kutoa ufadhili wa masomo kwa watu kutoka katika jamii zinazoishi katika Block 12A. Wanajamii walikuwa wanakusanyika na kuamua ni nani atakayepokea ufadhili wa masomo. Tullow iliongezea kuwa walitoa ufadhili wa masomo kwa watu walioathiriwa na miradi yao nchini Kenya. Hata hivyo, kwa kuzingatia ukubwa wa mradi wa Tullow katika eneo la Turkana ikilinganishwa na mradi katika Block 12A, ufadhili zaidi wa masomo ulitolewa kwa watu wa jamii za Turkana.

Tullow ilielezea CAO kuwa wanaweza kushiriki katika majadiliano na walalamishi yatakayoendeshwa na CAO, huku kukiwa na uwezekano wa Delonex kushiriki kama mwangalizi, iwapo wahusika watafikia makubaliano kuhusu kanuni zitakazotumika.

**KIAMBATISHO A. UTARATIBU UNAFUATWA NA CAO KUSHUGHULIKIA MALALAMISHI**

Punde baada za CAO kutangaza kuwa malalamishi yanakubalika, CAO, kupitia kwa wataalamu wake wa kutatua mizozo, hufanya tathmini ya mwanzo. Nia ya tathmini ya CAO ni: (1) kubainisha masuala na malalamishi yanayotolewa na mlalamishi/walalamishi; (2) kutafuta taarifa kutoka kwa washikadau wengine kupata maoni yao kuhusiana na hali hiyo; na (3) kuwasaidia washikadau kuelewa njia wanazoweza kutumia kutatua mzozo na kubainisha iwapo wangependa kushirikiana kutafuta suluhu kupitia Kitengo cha Kutatua Mizozo cha CAO, au iwapo kesi hiyo inapaswa kushughulikiwa upya na Kitengo cha Ridhaa cha CAO.

Kwa kuzingatia Mwongozo wa Utendaji Kazi wa CAO,[3] hatua zifuatazo hufuatwa ili kushughulikia malalamishi yaliopokelewa:

Hatua ya Kwanza: **Kukubali** kuwa malalamishi yamepokelewa.

Hatua ya Pili: **Kukubalika:** Kubainisha iwapo malalamishi yanakubalika kushughulikiwa na CAO (hii hufanyika kwa siku za kufanya kazi zisizozidi 15).

Hatua ya Tatu: **Tathmini ya CAO:** Kutathmini maswala yaliyoibuliwa na kuwasaidia washikadau kuyaelewa na kubainisha iwapo wangependa kushirikiana kupata suluhisho chini ya usaidizi wa kitengo cha CAO cha Kutatua Mizozo, au iwapo kesi hiyo inapaswa kushughulikiwa na kitengo cha Ridhaa cha CAO ili kuchunguza iwapo utaratibu wote wa kimazingira na kijamii unaotolewa na IFC's/MIGA umefuatwa kikamilifu. Mda wa kutathmini unaweza chukua siku za kufanya kazi zisizozidi 120.

Hatua ya Nne: **Kuwezesha usuluhishaji:** Iwapo wahusika watakubali kushirikiana kutatua mzozo, Kitengo cha CAO cha Kutatua Mizozo kitahusika. Mchakato wa utatuzi wa mzozo huzingatia au kufuata Mkataba wa Maafikiano na/au kutumia sheria zinazowekwa chini na kukubaliwa na makundi husika. Inawezahusisha kusaidiwa/upatanisho, kushirikiana kutafuta ukweli, au njia yoyote itakayokubaliwa inayoweza kuleta suluhisho au kusaidia kufikia malengo mwafaka yaliyowekwa kwa pamoja. Lengo kuu la kutumia njia hii kutatua mzozo ni kushughulikia masuala yanayojitokeza kwenye malalamishi, na masuala mengine yoyote muhimu yanayohusiana na malalamishi yaliyojitokeza wakati wa kutathmini mzozo au wakati wa mchakato wa utatuzi wa mzozo kwa njia inayokubalika kwa wahusika wote.[4]

AU

**Kutathmini kwa Ridhaa/Uchunguzi:** Iwapo wahusika watachagua mchakato wa Ridhaa, kitengo cha CAO cha Ridhaa kitaanza kutathmini iwapo utaratibu wote wa kimazingira na kijamii unaotolewa na IFC's/MIGA umefuatwa kikamilifu kuhusiana na mradi husika. Hii itasaidia kubainisha iwapo uchunguzi wa utendakazi wa IFC/MIGA kuhusiana na mradi una mashiko. Mda wa kutathmini unaweza kuchukua mda usiozidi siku za kufanya kazi 45. Uchunguzi ukipatikana kuwa na mashiko, kitengo cha CAO cha Ridhaa kitafanya uchunguzi wa kina unaohusu utendakazi wa IFC/MIGA. Ripoti ya uchunguzi ikijumuisha mambo yoyote

[3] Kwa maelezo zaidi kuhusiana na majukumu na kazi ya CAO, tafadhali soma mwongozo mzima wa utendakazi kwenye: http://www.cao-ombudsman.org/documents/CAOOperationalGuidelines_2013.pdf

[4] Pale ambapo washikadau watashindwa kutatua malalamishi kwa kushirikiana kwa mda uliowekwa, Kitengo cha CAO cha Utatuzi wa Mizozo kitatafuta kwanza kusaidia washikadau kukabiliana na changamoto. Iwapo haitawezekana, kikosi cha Utatuzi wa Mizozo kitaeleza washikadau, wakiwemo wafanyakazi wa IFC/MIGA, Rais na Bodi ya Benki ya Dunia, na umma, kuwa kikosi cha CAO cha Utatuzi wa Mizozo kimefunga malalamishi na kuyahamishia kitengo cha Ridhaa cha CAO kuyatathmimi.

yanayoonyesha kutoridhia itawekwa wazi, pamoja na hatua zilizochukuliwa na IFC/MIGA.

Hatua ya Tano: **Ufuatiliaji**

Hatua ya Sita: **Hitimisho/Kufungwa kwa kesi**